

Kliniki za Utoaji wa Chanjo ya Johnson & Johnson katika Vermont Kuanza Tena
Kulingana na matokeo ya CDC kwamba hatari ya kuganda kwa damu ni nadra sana

BURLINGTON, VT - Idara ya Afya ya Vermont ilitangaza kuwa itaanza tena kutumia chanjo za Johnson & Johnson. Uamuzi huu ulitolewa baada ya FDA na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) kutangaza kwamba kamati yake ya ushauri imebaini kuwa chanjo ni salama na yenye ufanisi kwa matumizi, na kwamba amri ya kusimamishwa ambayo imekuwapo tangu tarehe 13 Aprili inaweza kuondolewa.

“Tunafurahi kwamba chanjo hii inapatikana tena ili kulinda wakazi wa Vermont kutokana na virusi vya COVID-19,” alisema Kamishna wa Afya Mark Levine, MD. “Nahimiza kila mtu anayestahiki, apate chanjo haraka iwezekanavyo kadri inavyopatikana na inayofaa kwako.”

Wakazi wa Vermont walio na umri wa miaka 18 na zaidi wanaweza kujiandikisha sasa kwenye kliniki zinazotoa chanjo ya dozi moja ya Johnson & Johnson. **Ili kujiandikisha kuweka miadi, tembelea healthvermont.gov/MyVaccine. Ikiwa unahitaji msaada, piga simu 855-722-7878 na ubonyeze 1 kwa huduma za ukalimani.** Wakazi wa Vermont walio na umri wa miaka 16 na 17 wanastahiki chanjo ya Pfizer tu.

“Ingawa usimamishaji ulikuwa kwa bahati mbaya, lengo letu kuu ni kuhakikisha kwamba chanjo ni salama,” alisema Dk. Levine. “Kwa kuzingatia mtazamo wa afya ya umma, hatua zilizochukuliwa ili kusimamisha na kuchunguza zilikuwa sahihi kabisa – hivi ndivyo sayansi hutumika. Tuna jukumu la kuhakikisha kuwa watu wanaamini mchakato huu, pamoja na chanjo zote.”

Vermont iliungana na majimbo mengine mengi katika kusimamisha matumizi ya chanjo kutokana na mapendekezo ya CDC, baada ya taarifa za idadi chache za kuganda kwa damu miongoni mwa wapokeaji chanjo. Maafisa wa afya wa nchi walitangaza usimamishaji huu ili kuipa Kamati ya Ushauri wa Desturi za Chanjo ya CDC muda wa kukagua data ya ziada kuhusu athari zilizoripotiwa.

Dk. Levine alisema kuwa wakati wa usimamishaji, watoa huduma za afya wa Vermont walipewa maelezo na mwongozo kuhusu dalili zinazoweza kuganda damu na matibabu sahihi. Mwongozo uliosasishwa utaendelea kutolewa.

Karibu dozi milioni 8 za chanjo ya Johnson & Johnson zimetolewa nchini Marekani. Taarifa ambazo zilisababisha kusimamishwa kwa muda zilihusu aina nadra na kali ya kuganda kwa damu inayoitwa cerebral venous sinus thrombosis (CVST). Matatizo hayo yaligundulika wiki 2 baada ya kupata chanjo. Hakujakuwa na visa vilivyoripotiwa vya athari hizi katika Vermont.

Ingawa [athari](#) zinazotiliwa wasiwasi ni nadra sana, FDA na CDC wanapendekeza kwamba watu wanaopata maumivu makali ya kichwa, maumivu ya tumbo, maumivu ya miguu au upungufu wa pumzi ndani ya wiki tatu baada ya kupokea chanjo ya Johnson & Johnson wawasiliane [mara moja](#) na watoa huduma wao wa afya.